

Jina _____ Namba ya Mtahiniwa _____

1013/2

P1 KISWAHILI

Karatasi 2

P.T.E.

Julai/Agosti 2011

Muda: Saa 2 $\frac{1}{2}$

Sahihi ya Mtahiniwa _____

Tarehe _____



THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

PRIMARY TEACHERS EXAMINATION

KISWAHILI

Karatasi 2

Saa 2 $\frac{1}{2}$

MAAGIZO

Andika jina lako na namba yako kwenye nafasi uliyoachiwa.

Mtihani huu una sehemu MBILI muhimu: FASIHI na TARATIBU ZA KUFUNDISHIA.

Ni muhimu sana ufuata maagizo uliyopewa mwanzo wa kila sehemu.

Andika majibu yako kwenye nafasi ulizoachiwa.

Usitoe karatasi yoyote katika kijitabu hiki.

Kwa Matumizi ya mtahini

Sehemu	Swali	Upeo	Alama
1	1	15	
	2	15	
	3	15	
	4	15	
	5	15	
	6	15	
2	7	17	
	8	20	
	9	18	
Jumla			

Kijitabu hiki kina kurasa 16 zilizopigwa chapa.

Watahiniwa ni lazima wahakikisha kuwa kurasa zote za karatasi hii
zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

USHAIRI

Jibu swali la **kwanza** au la **pili**.

1. Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

S.A. MOHAMED. *Sikate Tamaa*

Jicho, tavumiliaje, kwa hayo uyaonayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo?
Kwacho, lijalo nalije, nimechoka yumiliyo
Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhi tusikiayo
Nayo, visa na mauko, wanyonge yawakutayo
Kwayo, sina zuiliko, natoa niyahisiyo
Naandika!

Hawa, wanetulimiya, dhiki wavumiliayo
Hawa, mamiya mamiya, na mali wazalishayo
Hawa, ndo wanoumiya, na maafa wakutayo
Naandika!

Hawa, sioni wengine, kwao liko angamiyo
Hawa, huwapa unene, watukufu wenyenay
Hawa, bado ni wavune, kwa shida waikutayo
Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenyenay pupa na kamiyo
Bado, tafauti sana, kwa pato na mengineyo
Bado, tuling'owe shina, ulaji pia na choyo
Naandika!

- (a) Kwa nini mshairi amechoka? Toa sababu **nne**.

(alama 4)

- (b) Andika bahari zinazojitekeza katika shairi hili ukizingatia:

(i) Mishororo _____

- (ii) Vipande _____
(iii) Kibwagizo _____ (alama 3)
(c) Toa mifano ya aina **mbili** za uhuru wa kishairi uliotumika katika shairi. (alama 2)

- (d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)

- (e) Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyonotumika kwenye shairi.
(i) Mauko _____
(ii) Wavune _____ (alama 2)

2. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

KING'EJ NA AMATA: *Taaluma ya Ushairi*

Kupenda mno ukwasi, naona nitapotea,
Mali ina wasiwasi, sikai nikatulia,
Mali huzua maasi, mtu **yakampotoa**.

Mwenye mali huzuzuka, kheri akaziambaa,
Na heshi kubabaika, kushukushuku jamaa,
Na huko kufilisika, akuhofu kila saa.

Maadui wa mkwasi, ni wengi kupindukia,
Rafikize si halisi, **ghalibu** humdowea,
Wamchomoe fulusi, kisha wamtete pia.

Kheri nikidhiwe haja, shida zikinifikia,
Nile kadiri ya haja, na nione njaa pia,
Na niipate faraja, dhiki zikinitokea.

He Mola wangu Bwana, Jalla wa ala Jalia,
Ufukara Maulana, nakuomba nepushia,
Nipe riziki mwanana, haja kunitoshelea.

Ukinipa utajiri, nipe na elimu pia,
Mali zangu niajiri, ziwaafalie insia,
Nikushukuru Qahari, vile kunifadhilia.

- (a) Kwa kutoa mifano **mitano** fafanua mtazamo wa mshairi kubusu mali. (alama 5)

- (b) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)

- (c) Toa mifano ya matumizi ya mbinu zifuatazo za lugha kwenye shairi.

- (i) Tashihisi _____
(ii) Takniri _____
(iii) Inkisari _____
(iv) Kufinyanga sarufi _____ (alama 4)

- (d) Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye shairi

- (i) *yakampotoa* _____
(ii) *ghalibu* _____ (alama 2)

TAMTHILIA

Jibu swali la Tatu au la Nne

3. K.W. WAMITILA: *Pango*

(a) ...“Raha hasa hii; nundu ya maisha bii! Wanajua kuandika kabisa hawa! Ehh ... Si neno, hiyo elim sina ... lakini? Kwani elimu ni nini humu mwetu? Ehh....”

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Andika na kutolea mifano mbinu **tatu** za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili.

(alama 3)

(b) “Suala la utetezi wa haki ni mojawapo ya maudhui yaliyoshughulikiwa na mwandishi.” Thibitisha. (alama 8)

4. KITHAKA WA MBERIA: *Natala*

“Chui halisi hawatangazi kucha zao ...kwa heri Tila”.

- (a) Fafanua muktagha wa dondoo hili. (alama 5)

- (b) Eleza umuhimu wa mzungumzaji katika tamthilia. (alama 10)

SEHEMU YA PILI:

MBINU ZA KUFUNDISHIA (alama 55)

Siba Maswali yote.

7. Eleza jinsi utakavyofunza somo la ufharnu katika darasa la tano. (alamu 17)

8. Fafanua jinsi nyenzo zifuatazo zinavyoweza kufanikisha ufunzaji katika darasa la saba:

- (a) Kamusi
- (b) Redio
- (c) Vifaa halisi
- (d) Maktaba

(alama 20)

9. Eleza malengo ya kijumla ya kufundisha mdahalo / mjadala katika darasa la saba.
(alama 18)